

## HALMASHAURI YA WILAYA YA SIHA



# **TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI**

Kumb. Na.SDC/B.20/7/68

27/08/2020

**MKURUGENZI MTENDAJI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA SIHA ANAWATANGAZIA  
WANANCHI WOTE WENYE SIFA KUOMBA NAFASI ZA KAZI ZIFUATAZO;-**

### **1. NAFASI YA KAZI : MTENDAJI WA KIJIJI DARAJA LA III - (NAFASI 1)**

#### **SIFA ZA MWOMBAJI:**

- Awe na Elimu ya Kidato cha Nne (IV) au Sita (VI)
- Aliyehitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti katika moja ya fani zifuatazo ;- Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha , Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa, kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

#### **KAZI NA MAJUKUMU:**

1. Kusimamia Ulinzi na Usalama wa raia na mali zao.
2. Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango ya Mendeleo ya Kijiji.
3. Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji.
4. Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji.
5. Kutafsiri na kusimamia sera, sheria na taratibu.
6. Kiongozi wa wakuu wa vitengo vya Kitaalamu katika Kijiji

7. Kuandaa Taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza uzalishaji mali.

#### **MSAHARA:**

- Ngazi ya mshahara wa Serikali ni **TGS B** kwa mwezi

#### **2. KATIBU MAHSUSI (III) - (NAFASI -1)**

- Awe na Elimu ya Kidato cha Nne (IV)
- Awe amehudhuria mafunzo ya uhazili na kufaulu mtihani wa Hatua ya tatu
- Awe amefaulu somo la Hatimkato ya Kiswahili na kiingereza maneno 80 kwa dakika 1
- Awe amepata mafunzo ya kompyuta kutoka chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali na kupata cheti katika program za Windows, Microsoft Office, Internet, E-mail na Publisher.

#### **KAZI NA MAJUKUMU:**

1. Kuchapa barua, taarifa na nyaraka za kawaida.
2. Kupokea wageni na kuwasaili shida zao na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa.
3. Kutunza taarifa /kumbukumbu za matukio, miadi na ratiba ya kazi nyingine.
4. Kupokea majalada, kuyagawa kwa Maofisa walio katika sehemeu alipo na kuyakusanya, kuyatunza na kuyarudisha sehemu zinazohusika.

#### **MSAHARA:**

- Ngazi ya mshahara wa Serikali ni **TGS B** kwa mwezi

#### **UTARATIBU WA KUTUMA MAOMBI**

1. Waombaji wote wawe ni raia wa Tanzania na wenye umri usiozidi miaka 45

2. Waombaji wote waambatishe na nakala za vyeti vya Elimu, Taaluma, Cheti cha Kuzaliwa na picha ndogo mbili za rangi (*passport size*)
3. Waombaji wote waambatanishe na maelezo binafsi yaliyojitosheleza (detailed C.V) yenye anuani na namba za simu.
4. Waombaji waliosoma nje ya Nchi, waambatanishe uthibitisho wa vyeti vyao kutoka Baraza la Mamlaka husika (**TCU na NECTA**)
5. Waombaji watakaokidhi sifa wataitwa kwenye usaili.
6. Waombaji watakaoitwa kwenye usaili watatakiwa waje na vyeti halisi (*Original Certificates*)

**NB:** Maombi yote yatumwe kwa anuani ifuatayo;-

**MKURUGENZI MTENDAJI,  
HALMASHAURI YA WILAYA YA SIHA,  
S.L.P 129,  
SIHA.**

Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe 24/09/2020 Saa tisa na nusu Alasiri  
(9:30)



Ndaki S. Mhuli

**MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA  
SIHA**